Kwanini Muislamu haruhusiwi kusherehekea maulidi?.

[Swahili- Kiswahili- سواحيلي]

Mtunzi:
Alhidaaya.com

Mfasiri:
Alhidaaya.com

Kimerejewa na:
Yunus Kanuni Ngenda.
Abubakari Shabani Rukonkwa.

لماذا لايحتفل المسلم بمولد النبي وغيرها من البدع والخرافات؟

المؤلف:

موقع الهداية

المترجم:

موقع الهداية

المراجع:

يونس كنون نغندا

أبوبكر شعبان ركونكوا.

بسم الله الرحمن الرحيم

Kwanini Muislamu haruhusiwi kusherehekea maulidi?.

AlhamduliLLaah - Sifa njema zote Anastahiki Allaah (Subhaanahu wa Ta’aala) Mola wa walimwengu wote, Swalah na salamu zimshukie kipenzi chetu Mtume Muhammad (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) na Swahaba zake (Radhiya Allaahu 'anhum) na waliowafuata kwa wema mpaka Siku ya Mwisho.

Zifuatazo ni sababu na hoja ambazo Muislam mwenye kupenda kufuata haki na mwenye kutaka apate uongofu ili abakie katika njia iliyonyooka na ajiepushe na mambo ya baatil. Hoja ni za wazi kutoka katika Qur-aan na Sunnah. Hoja za kupinga jambo hili ziko nyingi sana, lakini tulizozikusanya tunatumai kuwa zitamtosheleza Muislamu aikinaishe nafsi yake kuwa Maulidi ni jambo la uzushi katika dini kwa hiyo ni bora kutenda amali zile tulizopata mafundisho yake kutoka kwa Mtume (s.a.w), Maswahaba wake na Salafu Swaalih (Watu wema walio tangulia).

1- Sababu Ya Kwanza:

Kumpenda Mola Mtukufu Aliyetuumba

Kwanza kabisa ni kwa sababu ya kumpenda Mola Mtukufu Aliyetuumba Ambaye Anataka kuhakikisha kuwa mapenzi yetu ambaye tokea kuzaliwa Kwake ni kumfuata Mtume (s.a.w) kwake hadi kufa kwake hakufanyiwa wala hakusherehekea siku yake ya kuzaliwa.

Anasema Allaah Mtukufu:

((قُلْ إِن كُنتُمْ تُحِبُّونَ اللّهَ فَاتَّبِعُونِي يُحْبِبْكُمُ اللّهُ وَيَغْفِرْ لَكُمْ ذُنُوبَكُمْ وَاللّهُ غَفُورٌ رَّحِيمٌ
((

Sema: Ikiwa nyinyi mnampenda Allaah basi nifuateni mimi,)) Allaah Atakupendeni na Atakufutieni madhambi yenu. Na Allaah ni Mwenye kufuta madhambi na Mwenye kurehemu)).

[Al-'Imraan: 31]

2-Sababu Ya Pili:

Kufuata amri yake Mtume (s.a.w) ya kushikamana na Sunnah Zake na Sunnah za Makhalifa wake.

((أوصيكُمْ بِتَقْوى اللّه، وَالسَّمْعِ وَالطّاعَةِ وإنْ تَأمَّر عَلَيْكُمْ عَبْدٌ حبشيٌ ، وَأَنَّهُ مَنْ يَعِشْ مِنْكُمْ فَسَيَرى اخْتِلافاً كثِيرا . فَعَلَيْكُمْ بسُنَّتي وَسُنَّةِ الْخُلَفَاءِ الرّاشِدِينَ الْمَهْدِيِّينَ ، عضوُّا عَلَيْهَا بالنَّواجِذِ ، وإيّاكُمْ ومُحْدثَاتِ الأمُورِ فَإنّ كُلّ بِدْعَةٍ ضلالَةٌ))

رواه أبو داود ، والترمذِي وقال حديث حسن صحيح

((Nakuusieni kumcha Allaah, usikivu na twaa hata ikiwa kiongozi wenu (Au atakayekuamrishen) ni Mtumwa wa Habash. Mtakaoishi miongoni mwenu mtaona ikhtilafu nyingi. Kwa hiyo shikamaneni na Sunnah zangu na Sunnah za Makhalifa waliongoka baada yangu. Ziumeni kwa magego (zikamateni kwa nguvu wala msiziache). Na tahadharini na mambo ya uzushi kwani kila bid'ah ni upotofu).

[Abu Daawuud, At-Trimidhiy kasema Hadiyth Hasan Swahiyh].

Kwa hiyo inamtosheleza Muislamu hoja hii pekee ya kuwa Mtume (s.a.w) wala Maswahaba zake hawakusherehekea Maulidi, kumfanya naye asisherehekee.

Na hiyo ndiyo sababu kubwa ya Waislamu kukhitilafiana na kugawanyika makundi makundi.

Amesema Imaam Maalik (r.h): "Hakunakitakachotengeneza Ummah huu wa mwisho ila kwa kile kilichotengeneza Ummah wa mwanzo".

Na maadam Salafus-Swaalih (wema waliotangulia) hawakufanya bid'ah kama hii, sisi ni lazima tuwe na khofu kubwa ya kuifanya.

3-Sababu Ya Tatu:

Ametuamrisha Allaah Mtukufu tufuate aliyotuletea Mtume (s.a.w), na tujiepushe na aliyotukataza.

((وَمَا آتَاكُمُ الرَّسُولُ فَخُذُوهُ وَمَا نَهَاكُمْ عَنْهُ فَانتَهُوا))

((Na anachokupeni Mtume chukueni, na anacho kukatazeni jiepusheni nacho)) [Al-Hashr: 7].

4-Sababu Ya Nne:

Kufuata amri ya Kumtii Allaah na Mtume wake (s.a.w).

Anasema Allaah Mtukufu katika Aayah nyingi ndani ya Qur-aan Tukufu:

((وَأَطِيعُوا اللَّهَ وَأَطِيعُوا الرَّسُولَ))

((Na mtiini Allaah na mtiini Mtume)) [At-Taghaabun: 12]

Na kumtii Allaah ni kumtii Mtume (s.a.w)

((مَّنْ يُطِعِ الرَّسُولَ فَقَدْ أَطَاعَ اللَّهَ))

((Mwenye kumtii Mtume basi ndio amemtii Allaah)) [An-Nisaa: 80].

5-Sababu Ya Tano:

Kutokufuata amri ya Mtume (s.a.w) ni kumkhalifu na kupata adhabu kali.

((فَلْيَحْذَرِ الَّذِينَ يُخَالِفُونَ عَنْ أَمْرِهِ أَن تُصِيبَهُمْ فِتْنَةٌ أَوْ يُصِيبَهُمْ عَذَابٌ أَلِيمٌ))

((Basi nawatahadhari wanaokhalifu amri yake, usije ukawapata msiba au ikawapata adhabu chungu)) [An-Nuur: 63].

6-Sababu Ya Sita:

Kumpinga Mtume (s.a.w) ni sababu ya kuingizwa motoni.

((وَمَن يُشَاقِقِ الرَّسُولَ مِن بَعْدِ مَا تَبَيَّنَ لَهُ الْهُدَى وَيَتَّبِعْ غَيْرَ سَبِيلِ الْمُؤْمِنِينَ نُوَلِّهِ مَا تَوَلَّى وَنُصْلِهِ جَهَنَّمَ وَسَاءَتْ مَصِيرًا))

((Na anayempinga Mtume baada ya kumdhihirikia uongofu, na akafuata njia isiyo kuwa ya Waumini, tutamuelekeza alikoelekea, na tutamuingiza katika Jahannamu. Na hayo ni marejeo maovu)) [An-Nisaa: 115].

7-Sababu Ya Saba:

Kuogopa upotovu unaompeleka mtu motoni Mtume (s.a.w) Alikuwa akitanguliza khutba zake kwa kutoa maonyo hayo:

((إن خير الكلام كلام الله وخير الهدي هدي محمد صلى الله علي وسلم وشر الأمور محدثاتها وكل محدثة بدعة وكل بدعة ضلالة وكل ضلالة في النار)) أخرجه مسلم في صحيحه.

((Maneno bora ni kitabu cha Allaah (Qur-an) na Uongofu bora kabisa ni uongofu wa Muhammad (s.a.w) na jambo la shari kabisa ni uzushi, na kila uzushi (katika dini) ni bid'ah (uzushi) na kila bid'ah ni motoni))

[Muslim katika Swahiyh yake]

8-Sababu Ya Nane:

Khofu ya kuwa miongoni mwa kundi litakaloingia motoni, alipoonya katika Hadithi ifuatayo kuwa makundi Mtume (s.a.w) yote yanayojiita ni ya Kiislam na hali hayafuati mafunzo kama aliyokuja nayo yeye, yatakuwa motoni isipokuwa kundi moja. Maswahaba walishituka na wakataka kujua ni kundi gani hilo moja, akawajibu kuwa ni kundi ambalo watu wake watakuwa wanafuata mwendo wake na wa Maswahaba zake.

((افترقت اليهود على إحدى وسبعين فرقة، وافترقت النصارى على اثنتين وسبعين فرقة، وستفترق هذه الأمة على ثلاث وسبعين فرقة كلها في النار إلا واحدة،))

فقال الصحابة : من هي يا رسول الله؟ قال: ((من كان على مثل ما أنا عليه وأصحابي)) الترمذي و الحاكم

((Waligawanyika Mayahudi katika makundi sabini na moja, na waligawanyika Manaswara katika makundi sabini na mbili, na utagawanyika Umma wangu katika makundi sabini na tatu, yote

yataingia motoni ila moja!)) Maswahaba wakasema: 'Ni kundi lipi hilo Ee Mtume wa Allaah? Akajibu: ((Ni lile ambalo litakuwa katika mwenendo wangu hii leo na Maswahaba zangu)).

Imepokewa na Maimaam At-Tirmidhiy na Al-Haakim].]

9-Sababu Ya Tisa:

Kuitikia wasiya wa Allaah ili kubakia katika njia iliyonyooka

Anasema Allaah Mtukufu:

((وَأَنَّ هَذَا صِرَاطِي مُسْتَقِيمًا فَاتَّبِعُوهُ وَلاَ تَتَّبِعُواْ السُّبُلَ فَتَفَرَّقَ بِكُمْ عَن سَبِيلِهِ ذَلِكُمْ وَصَّاكُم بِهِ لَعَلَّكُمْ تَتَّقُونَ))

((Na kwa hakika hii ndiyo Njia Yangu Iliyonyooka. Basi ifuateni, wala msifuate njia nyingine, zikakutengeni na Njia yake. Haya Amekuusieni ili mpate kumcha Mungu)) [Al-An'aam: 15]

10-Sababu Ya Kumi:

Vitendo visivyokuwa vya Sunnah havipokelewi

((من عمل ليس عليه أمرنا فهو رد)) البخاري

((Atakayetenda kitendo kisichokuwa chetu (katika dini yetu) basi kitarudishwa)) [Al-Bukhaariy].

Hivyo mtu atapoteza muda wake, labda na gharama ya kutekeleza bid'ah hii na kumbe amali hii haina thamani yoyote mbele ya Allaah.

11-Sababu Ya Kumi Na Moja:

Maulidi yamezushwa karne ya nne (miaka mia nne) baada ya kufa Mtume (s.a.s) na watu wenye kufru.

Walioanzisha Maulidi ni viongozi wa Faatwimiyyun huko Misr (hawa walikuwa ni Rawaafidh (Mashia) katika dhehebu la Ismailiyah [Makoja] walianza kusherehekea Maulidi ya ‘Aliy bin Abi Twaalib (Radhiya Allaahu ‘anhu), na Maulidi ya Hasan na Husayn (Radhiya Allaahu ‘anhuma), na Maulidi ya Faatwimah az-Zahraa (Radhiya

Allaahu ‘anha), na Maulidi ya kiongozi wao aliye hai kwa wakati ule. Sasa kwa nini tuwafuate wao? Na kama alivyotujulisha Mtume (s.a.w) kwamba watu bora kabisa wa kuwafuata ni wa karne tatu pekee aliposema:

((خير القرون قرني ثم الذين يلونهم ثم الذين يلونهم)) متفق عليه

((Karne zilizo bora kabisa ni karne yangu, kisha inayofuatia kisha inayofuatiya)) [Al-Bukhaariy na Muslim]

12-Sababu Ya Kumi Na Mbili:

Makafiri wanafurahi Waislamu wanapofanya Bid'ah kwani ni kuacha mafunzo sahihi ya dini na ni kuzifuta Sunnah za Mtume (s.a.w).

Napoleon Bonaparte alimpa Shaykh Al-Bakriy Riyaal mia nane za Ufaransa (inasemekana ni mia tatu kwenye sehemu zingine) ili arudishe bid'ah ya Maulidi naye akahudhuria mwenyewe Maulidi. Maana makafiri wanajua kuwa Waislam wanaposhughulishwa na vipumbazo kama hivyo, husahau matakwa yao ya msingi na muhimu.

13-Sababu Ya Kumi Na Tatu:

Baadhi ya maneno katika Maulidi yana kufru ya kumpandisha Mtume (s.a.w) cheo cha usawa na Allaah Mtukufu wakati yeye ametuonya tusifanye hivyo

((لا تطروني كما أطرت النصارى المسيح ابن مريم، إنما أنا عبد، فقولوا: عبد الله ورسوله)) متفق عليه

((Msinitukuze Kama Manaswara walivyomtukuza Masiyh mwana wa Maryam, hakika mimi na mja kwa hiyo semeni mja wa Allaah na Mjumbe Wake)) [Al-Bukhaariy na Muslim]

14-Sababu Ya Kumi Na Nne:

Wanapoinuka kumswalia Mtume (s.a.w) wanaamini kwamba roho yake inahudhuria wakati huo

Hii ni itikadi ovu kabisa, na pia yeye mwenyewe alikuwa hapendi kuinukiwa alipokuwa hai, vipi mtu anayempenda amfanyie jambo analolichukia wakati amekufa?

Siku moja Maswahaba walikuwa wamekaa msikitini pamoja na Abubakar (r.a) ambaye alikuwa akisoma Qur-aan. 'Abdullah ibn Ubbay ibn Saluul, mnafiki mkubwa alikuja akaweka takia na mto wake akaketi. Alikuwa ni mwenye sura nzuri na mwenye lugha ya ufasaha. Alisema: "Ewe Abu Bakar, muulize Mtume (s.a.w) atuonyeshe alama ya utume wake kama walivyotuonyesha Watume wengine. Mfano, Muusa (a.s) ametuletea Ubao (wa Tauraat), 'Issa (a.s) alituletea Injiyl na meza ya chakula kutoka mbinguni, Daawuud (a.s) alituletea Zabuur, Swaalih (a.s) alitulietea ngamia wa kike" Abu Bakar (r.a) aliposikia akaanza kulia. Mara akaingia Mtume (s.a.w) na Abu Bakar (r.a) akawaambia Maswahaba wengine wainuke kumpa heshima Mtume (s.a.w) na kumpa malalamiko ya mnafiki. Mtume (s.a.w) akasema: ((Sikizeni! Msiniinukie mimi bali….

وَقُومُواْ لِلّهِ قَانِتِينَ

((na simameni kwa ajili ya Allaah)) [Al-Baqarah: 238] (dalili kutoka Tafsiyr Ibnu Kathiyr]

15-Sababu Ya Kumi Na Tano:

Kuchanganyika kwa wanawake na wanaume

Jambo ambalo limekatazwa katika dini na katika sherehe hii kumedhihirika sana hasa pande za nchi zetu za Afrika Mashariki. Na uovu huu unafikia hadi kuimba kwa pamoja na kuchezesha vichwa kama kwamba ni dansi fulani. Imefika hadi maulidi kuitwa ‘disco maulidi’

16-Sababu Ya Kumi Na Sita:

Kuwaigiza Manaswara

Manaswara wanasherehekea siku ya kuzaliwa 'Issa (a.s) kama wanavyodai. Na Waislamu haitupasi kusherehekea siku ya kuzaliwa Mtume (s.a.w) kwani tumefundishwa kuwa tufanye kinyume na wao katika mambo yetu.

Vilevile Mtume (s.a.w) kasema:

((خالفوا المشركين، أحفوا الشوارب، وأوفوا اللحى)) البخاري و مسلم

((Kuweni kinyume na Washirikina, punguzeni masharubu na fugeni ndevu)) [Al-Bukhaariy na Muslim]

Na kufanya hivyo (kusherehekea Maulidi) tutakuwa tunajifananiza nao, na jambo hilo la kuwaiga na kujifananisha na mambo yao limekatazwa kama alivyosema Mtume (s.a.w).

((من تشبه بقوم فهو منهم)) أحمد و أبو داود

Anayejishabihisha na watu basi naye ni miongoni mwao)) [Ahmad, Abu Daawuud]

17-Sababu Ya Kumi Na Saba:

Dini imekamilika hakuna tena haja ya kuleta mambo ya dini mapya

Kuzusha mambo mapya ya dini ni kama kumtuhumu Mtume (s.a.w) kuwa ametukhini mafunzo ya dini na hakuyakamilisha, bali kuna aliyoyaficha na hakutupa yote!! Na hali aliikamilisha dini kama ilivyompasa. Aayah hii chini iliteremshwa kudhihirisha ukamilifu wa dini ya Mola Mtukufu

((الْيَوْمَ أَكْمَلْتُ لَكُمْ دِينَكُمْ وَأَتْمَمْتُ عَلَيْكُمْ نِعْمَتِي وَرَضِيتُ لَكُمُ الإِسْلاَمَ دِينً))

((Leo Nimekukamilishieni Dini yenu, na nimekutimizieni Neema Yangu, na Nimekupendeleeni UISLAMU uwe ndiyo Dini)) [Al-Maaidah: 3]

Sasa vipi watu walete mafundisho ya dini mapya yasiyotokana na mafunzo kutoka kwa Allaah Mtukufu na Mtume Wake (s.a.w) Anauliza Allaah Mtukufu:

((أَمْ لَهُمْ شُرَكَاء شَرَعُوا لَهُم مِّنَ الدِّينِ مَا لَمْ يَأْذَن بِهِ اللَّهُ))

((Au hao wana miungu ya kishirikina waliowatungia dini asiyoitolea idhini Allaah?)) [Ash-Shuura 21]

18-Sababu Ya Kumi N a Nane:

Kudhihirisha imani kwa kupenda yale aliyokuja nayo Mtume (s.a.w) pekee.

عَنْ أَبِي مُحَمَّدٍ عَبْدِ اللَّهِ بِنْ عَمْرُو بِنْ العَاصِ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا قَالَ : قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صلى الله عليه وآله وسلم: ((لا يُؤْمِنُ أَحَدُكُمْ حَتَّى يَكُونَ هَوَاهُ تَبَعاً لِمَا جِئْتُ بِهِ)) حَدِيثٌ حَسَنٌ صَحِيحٌ، رَوَيْنَاهُ فِي كِتَابِ "الْحُجَّةِ بِإِسْنَادٍ صَحِيحٍ.

Kutoka kwa Abu Muhammad Abdullah Ibn 'Amr Bin Al-'Aasw (r.a) ambaye alisema: Mtume (s.a.w) kasema: ((Hatokuwa kaamini (kikwelikweli) mmoja wenu mpaka mapenzi yake yatakapomili (yatakapotii au kuwafikiana) kwenye yale niliyoyaleta)) (mafundisho) [Hadiyth Hasan iliyotoka katika kitabu “Al-Hujjah” ikiwa na mtiriko mzuri wa mapokezi].

19-Sababu Ya Kumi Na Tisa:

Kuacha mambo yenye shaka na kubakia katika yaliyo wazi

عَنْ أَبي مُحمَّدٍ الحسَنِ بْنِ عليّ بْنِ أبي طَالِب، سِبْطِ رَسُولِ اللهِ صلى الله عليه وسلم وَرَيْحَانَتِهِ رضيَ اللهُ عنهُما، قالَ: حَفِظْتُ مِنْ رَسُولِ الله صلى الله عليه وسلم: ((دَعْ ما يَرِيبُكَ إلى مَا لاَ يَرِيبُكَ)) رَوَاهُ التِّرْمِذِيُّ وَالنَّسَائِيُّ وَقَالَ التِّرْمِذِيُّ: حَدِيثٌ حَسَنٌ صَحِيحٌ.

Kutoka kwa Abu Muhammad Al-Hasan Ibn ‘Aliy Ibn Abi Twaalib mjukuu wa Mtume (s.a.w) na kipenzi chake (r.a) alisema: "Nilihifadhi kutoka kwa Mtume (s.a.w) maneno haya: ((Acha kile kinachokutia shaka ufuate kile kisichokutia shaka)). [Imesimuliwa na At-Tirmidhiy na An-Nasaaiy, At-Tirmidhiy akisema kuwa ni hadiyth Hasan na Swahiyh].

20-Sababu Ya Ishirini:

Mwezi huu wa Rabiy'ul Awwal ni mwezi alioaga dunia Mtume (s.a.w) sasa vipi Muislamu asherehekee?

Wanachuoni wote wameafikiana kuwa siku hii ya tarehe 12 Rabiy‘ul Awwal ni siku aliyofariki Mtume (s.a.w) Vipi sasa watu watakuwa wanafurahi kwa siku kama hiyo? Anas bin Maalik (r.a) anatuhadithia kuwa: "Hakuna siku ambayo watu wa Madiynah walikuwa na furaha ya hali ya juu kama siku aliyohamia Mtume (s.a.w) katika mji huo. Na hakuna siku ya huzuni kabisa kwa watu wa Madiynah kama siku aliyoaga dunia Mtume (s.a.w).

Inaonekana kama sisi tunakwenda kinyume na maadili ya wale watu bora waliokuwa wakimpenda Mtume (s.a.w) hata kuliko nafsi zao wenyewe.

21-Sababu Ya Ishirini Na Moja:

Sababu za Waislamu wanaoshikilia Bid'ah

1- Kufuata bila ya kupata elimu sahihi

Ukitaka kujua hoja za Waislamu wanaofuata bid'ah, hutopata kutoka kwao hoja nyingi kutoka katika Qur-aan na Sunnah, bali ni hoja za kutokana na rai zao tu, au watakwambia, 'kwani kuna ubaya gani?'. Na hata wakitoa hoja kutoka katika Qur-aan na Sunnah basi utakuta kwamba wanazifasiri dalili hizo isivyokusudiwa bali wanazishabihisha na matamanio yao kama Anavyosema Allaah Mtukufu:

((هُوَ الَّذِيَ أَنزَلَ عَلَيْكَ الْكِتَابَ مِنْهُ آيَاتٌ مُّحْكَمَاتٌ هُنَّ أُمُّ الْكِتَابِ وَأُخَرُ مُتَشَابِهَاتٌ فَأَمَّا الَّذِينَ فِي قُلُوبِهِمْ زَيْغٌ فَيَتَّبِعُونَ مَا تَشَابَهَ مِنْهُ ابْتِغَاء الْفِتْنَةِ وَابْتِغَاء تَأْوِيلِه))

((Yeye Ndiye Aliyekuteremshia Kitabu (hiki Qur-aan). Ndani yake zimo aayah Muhkam (nyepesi kufahamika) ambazo ndizo msingi (asili) wa Kitabu (hiki). Na ziko nyingine Mutashaabihaat (zinababaisha kama habari ya Akhera, za Peponi na Motoni na mengineyo ambao yamekhusika na Roho). Wale ambao nyoyoni

mwao mna upotofu wanafuata zile zinazobabaisha kwa kutaka kuwaharibu watu na kutaka kujua hakika yake vipi)) [Al-'Imraan: 7]

Na ukizingatia utaona kuwa Waislamu wanaofuata Bid'ah sio wenye elimu ya juu, kwani ukilinganisha na wanaofuata Sunnah utaona kuwa kuna tofauti kubwa sana. Na hivyo ndivyo Allaah Mtukufu Anavyomjaalia kumpa elimu ya upeo yule mwenye kufuata haki. Na tujiulize Maulamaa wangapi wacha Mungu wenye elimu madhubuti wanafuata Bid'ah? Si rahisi kuwapata, bali ukiuliza wanaofuata Sunnah na wenye elimu kubwa ambayo athari yake tunaiona leo hii na itaendelea kizazi hadi kizazi In Shaa Allaah, utakuta ni wengi sana, miongoni mwao ni Maimamu wanne; Imaam Shaafi'iy, Ahmad bin Hanbali, Abu Haniyfah, Maalik, Sufyaan Ath-Thawry. Wasimulizi wa Hadiyth kina Al-Bukhaariy, Muslim, Abu Daawuud, At-Tirmidhiy, An-Nasaaiy, Ibn Maajah na kadhalika. Maulamaa maarufu; Ibn Taymiyah, ibnul Qayyim, ibnul Jawzy, ibnul Mubaarak, ibnu Hajar, ibnu Kathiyr, Imaam An-Nawawy, na waliopita katika miaka ya karibuni kama kina: ibn 'Uthaymiyn, ibn Baaz, Shaykh Al-Albaaniy na kadhalika. Hata katika jamii yetu kuna waliokuwa wamejaaliwa kupewa kipaji cha elimu kama kina Shaykh 'Abdullah Swaalih Al-Faarisy na kina Al-Amiyn na Muhammad Qaasim Mazrui, Haarith Swaalih na wengineo wengi, bila kuwataja walio hai ambao hawana idadi kwa wingi wao.

2- Kufuata matamanio ya nafsi

Hufuata matamanio ya nafsi inavyopenda na sio kufuata haki. Wengine kutokana na unasaba wao huwa ni kwao kama utukufu kuwa nao wamo katika unasaba wa Mtume (s.a.w).

Anasema Allaah Mtukufu:

((وَلاَ تَتَّبِعِ الْهَوَى فَيُضِلَّكَ عَن سَبِيلِ اللَّهِ))

((Wala usifuate matamanio yakakupoteza kwenye Njia ya Allaah)) [Swaad: 26]

3- Ugumu wa kuacha mila uliotokana na mababa na mababu

Mitume waliopita walikuwa wakiwaita watu wao wawafuate waliyokuja nayo ya haki walipendelea kubakia katika ujinga na mila za mababa zao. Na Waislamu wenye kufuata mambo ya bid'ah nao ni vile vile ukiwauliza kwa nini hamuachi mambo yasiyo katika mafundisho ya Mtume (s.a.w) wanajibu hivyo hivyo kuwa 'vipi tuache Maulidi na hali tumekulia nayo?, au tutaachaje kitu ambacho mababa zetu walikuwa wakifanya?? Ina maana wao walikuwa hawajui?"

Anasema Allaah Mtukufu:

((وَإِذَا قِيلَ لَهُمْ تَعَالَوْاْ إِلَى مَا أَنزَلَ اللّهُ وَإِلَى الرَّسُولِ قَالُواْ حَسْبُنَا مَا وَجَدْنَا عَلَيْهِ آبَاءنَا أَوَلَوْ كَانَ آبَاؤُهُمْ لاَ يَعْلَمُونَ شَيْئًا وَلاَ يَهْتَدُون))

((Na wanapoambiwa: Njooni kwenye yale Aliyoyateremsha Allaah, na kwa Mtume, husema: Yanatutosha tuliyowakuta nayo baba zetu. Je, hata ikiwa baba zao walikuwa hawajui kitu wala hawakuongoka?)) [Al-Maaidah: 104]

Au walikuwa wakisema:

((بَلْ قَالُوا إِنَّا وَجَدْنَا آبَاءنَا عَلَى أُمَّةٍ وَإِنَّا عَلَى آثَارِهِم مُّهْتَدُونَ))

((Bali wanasema: Hakika sisi tuliwakuta baba zetu wanashika dini makhsusi, basi na sisi tunafuata nyayo zao))

[Az-Zukhruf: 22]

4- Kukhofu kutokuungana na wengi wanaofuata bid'ah

Wengine ukiwauliza kwa nini unafuata bid'ah ya Maulidi. Jibu ni kuwa anakhofu kuwa yeye peke yake ataonekana kuwa hasomi Maulidi katika kundi lake, na hii ni hatari ya kukhofu watu badala ya kumkhofu Mola Mtukufu na pia ni kwenda na mkumbo kwa kudhani kuwa wengi ndiyo wenye haki! Haya Anatueleza Allaah kuwa:

((وَإِن تُطِعْ أَكْثَرَ مَن فِي الأَرْضِ يُضِلُّوكَ عَن سَبِيلِ اللّهِ إِن يَتَّبِعُونَ إِلاَّ الظَّنَّ وَإِنْ هُمْ إِلاَّ يَخْرُصُونَ))

((Na ukiwatii wengi katika hawa waliomo duniani watakupoteza na Njia ya Allaah. Hawa hawafuati ila dhana tu, na hawakuwa ila ni wenye kusema uwongo tu)) [Al-An'aam: 116]

5- Wengine wanasema kuwa ni kudhihirisha mapenzi ya Mtume (s.a.w).

Je, mapenzi ya Mtume (s.a.w) yadhihirike siku moja tu? Au katika mwezi huu tu? Na si siku zote? Hayo bila shaka ni mapenzi ya uongo. Mapenzi ya kweli ni yale ya kumkumbuka siku zote na kumtii umpendaye. Haya ya Maulidi hayana moja kati ya mawili hayo.

6- Hoja ya kusema ni Bid'atun-hasanah (uzushi mzuri)

Mojawapo yao ni kuwa Maulidi ni Bid'atun-hasanah. Katika dini ya Kiislamu hakuna bid'ah nzuri kwani Mtume (s.a.w) alipotuonya alisema 'Kullu Bid'atin Dhwaalaah' (kila bid'ah ni upotofu). Na ikiwa kauli hii wanaipinga kuwa sio KILA bid'ah, basi wanasemaje kuhusu kauli ya Allaah Mtukufu Anaposema:

((كُلُّ نَفْسٍ ذَآئِقَةُ الْمَوْتِ))

((Kila nafsi itaonja mauti)) [Al-'Imraan: 185]

Je, tupinge pia kauli hii kuwa sio kila nafsi? Na je, ina maana kuwa kuna watu wengine watabakia hawatokufa na hali tunatambua kuwa hakuna atakayebakia ila Mwenyewe Mola Mtukufu?

Mwisho:

Kuna maswali machache ambayo anatakiwa kuyajibu mtu mwenye kusherehekea kuzaliwa mtume (s.a.w):

1.Nimara ngapi alisherehekea mtume siku ya uzao wake?

2.Ni sehemu gani maswahaba walisherehekea malidi?

3.Nichakula gani walicho kula wakisherehekea maulidi wakati wa sherehe ya maulidi?

4.Ni nashiidi au nyimbo walikuwa wakiimba wakati wakisherehekea Maulidi?.

TNB: Majibu ya maswali haya yanatakiwa yatolewe katika Quraan na Sunna sahihi za mtume (s.a.w), au katika Athari za Maswahaba (r.a) na Mataabii walio kuja baada ya maswahaba.

Ikiwa hauta pata majibu ya maswali haya jiulize wanao sherehekea wamepata wapi? Na iliwafikia vipi? Huo ndio Uzushi katika dini ya Mwenyezi Mungu.

Tunamuomba Allaah Mtukufu atuongoze kwa kutuonyesha yaliyo haki ili tuyafuate na Atuonyeshe yaliyo baatil tujiepushe nayo. Aamiyn.

MASWALI KABLA YA KUSOMA.

1: Kuna malengo gani kwenye ujumbe huu mmoja?

2: Kinasemaje kitabu kitakatifu kuhusu hilo?

3: Qur-an inasemaje kuhusu hilo?

4: Ipi rai yako baada ya hapo?

KIINI CHA MADA:

Baada ya kuumbwa Adam (s.a.w), ujumbe mmoja wamepewa watu karne na karne, kuna umuhimu wa kuwakumbusha watu ujumbe huu na kuwaweka katika njia iliyo nyooka, amewatuma Mwenyezi Mungu mmoja wa kweli Manabii na Mitume kama vile Adam, Nuuh, Ibrahim, Mussa, Issa na Muhammad (s.a.w), ili wafikishe ujumbe mmoja nao ni: (Mungu wa kweli ni mmoja tu muabuduni).

Mungu mmoja wa kweli ndiye (Muumbaji) na ndiye muabudiwa.

Amemtuma Mtume	Afikishe ujumbe huu
Nuuh (s.a.w)	Mungu ni mmoja muabuduni Mwenyezi Mungu
Ibrahim (s.a.w)	Mungu ni mmoja muabuduni Mwenyezi Mungu
Mussa (s.a.w)	Mungu ni mmoja muabuduni Mwenyezi Mungu
Issa (s.a.w)	Mungu ni mmoja muabuduni Mwenyezi Mungu
Muhammad (s.a.w)	Mungu ni mmoja muabuduni Mwenyezi Mungu

Kwa hakika Mwenyezi Mungu ametuma Mitume wastahamilivu na wengineo tunaowajua na tusiowajua miongoni mwa Manabii wake na Mitume wake, ili watekeleze mambo mengi yakiwemo:

1: Kupokea wahyi wa Mwenyezi Mungu na kuwafikishia watu wao na wafuasi wao.

2: Kuwafundisha watu tauhidi na kutakasa ibada zao kwa ajili ya Mwenyezi Mungu.

3: Wawe ndio kiigizo chema kwa kauli na matendo ili watu wawaige katika njia ya kuelekea kwa Mwenyezi Mungu.

4: Kuwaelekeza wafuasi wao namna ya kumuogopa Mwenyezi Mungu na kumtii na kufuata amri zake.

5: Kuwafundisha wafuasi wao mambo ya dini na tabia njema.

6: Kuwaongoza wafanyao maasi na washirikina wanaoabudu masanamu na wengineo.

7: Kuwaambia watu ya kwamba watafufuliwa baada ya kufa kwao na watahesabiwa siku ya kiyama kutokana na matendo yao, atakayekuwa amemuamini Mwenyezi Mungu peke yake na akafanya matendo mema malipo yake ni pepo, na yeyote atakae mshirikisha Mwenyezi Mungu na akamuasi mafikio yake ni motoni.

Kwa hakika Manabii hao na Mitume hao amewaumba na amewatuma Mungu mmoja tu.

Kwa hakika ulimwengu na viumbe vilivyomo vinakubali kuwepo Mungu muumbaji na vinashuhudia kuwa Mwenyezi Mungu ni mmoja tu, Mwenyezi Mungu ndiye aliyeumba ulimwengu na vilivyomo miongoni mwa binadamu na wanyama na wadudu. Naye ndiye aliyeumba kifo na uhai wenye kumalizika na maisha ya milele.

Kwa hakika vitabu vitakatifu upande wa Mayahudi na Manaswara vyote vinashuhudia uwepo wa Mwenyezi Mungu na kumpwekesha.

Kwa hakika yule anaetafuta haki atakapo soma maana ya Mungu kwa kina na ukweli kabisa katika vitabu vitakatifu na Qur-an Tukufu ataweza kupambanua sifa maalum zinazo muhusu Mwenyezi Mungu bila ya kushirikiana na miungu ya uongo. Na hizi ni baadhi ya sifa:

1: Mwenyezi Mungu wa kweli ndiye muumbaji na siyo kiumbe.

2: Mwenyezi Mungu wa kweli ni mmoja hana mshirika, na siyo zaidi ya mmoja hakuzaa wala hakuzaliwa.

3: Mwenyezi Mungu ni mwenye kutakasika kutokana na taswira ya viumbe, hadirikiwi (haonekani) na macho hapa duniyani.

4: Mwenyezi Mungu ni wa enzi, hafi wala hajitokezi au kujifananisha na maumbile ya viumbe vyake.

5: Mwenyezi Mungu ndiye mwenye kutegemewa na viumbe mwenye kujiendesha, mwenye kujitosheleza na viumbe wake, havihitajii hana mzazi wa kike wala wa kiume wala mke wala mtoto, hahitaji kula wala kunywa wala msaada wa yeyote. Lakini viumbe vilivyoumbwa na Mwenyezi Mungu ni vyenye kumuhitaji.

6: Mwenyezi Mungu ni mwenye kutakasika kwa sifa za ukamilifu asizo shirikiana wala kushabihiana na yeyote katika viumbe wake, hakuna anaye fanana nae.

Na yawezekana kutumia sifa hizi na sifa nyinginezo zinazo muhusu Mwenyezi Mungu peke yake katika kfichua na kupinga miungu yote inayodaiwa ya uongo.

Na sasa niacheni narudi kwenye ujumbe mmoja uliotajwa hapo juu ili nichukue baadhi ya dalili kutoka katika kitabu kitakatifu na Qur-an Tukufu zinazo tilia mkazo ya kuwa Mwenyezi Mungu ni mmoja. Na kabla ya yote napenda nikushirikisheni katika fikra hii: "Kuna baadhi ya wakristo wanadai kwamba Mungu ni mmoja na wao wanamwamini Mungu mmoja"

Na ukweli uliopo katika kusoma kwangu sana kuhusu ukristo na mjadala pamoja na wakristo nimekuta kwamba "Mwenyezi Mungu" kwa upande wao anafungamana na mambo yafuatayo:

1: Mungu Baba.

2: Mungu Mwana.

3: Mungu Roho Mtakatifu.

Kwa hakika kwa maumbile ya kawaida na akili iliyokuwa safi inampelekea mpekuzi wa mada hii kuwauliza maswali mengi wakristo:

Nini maana yenu kusema ya kwamba "Mungu ni mmoja" wakati nyinyi mnaashiria miungu watatu?

Je! Mwenyzi Mungu ni mmoja kagawanyika katika utatu au utatu umekuwa kitu kimoja (1 katika 3 au 3 katika 1)?

Ukijumlisha hayo na ukizingatia itikadi ya baadhi ya wakristo kwamba miungu hawa watatu wana kazi maalum wana sifa maalum na namna maalum kama ifuatavyo:

1: Mungu Baba = ndiye muumbaji.

2: Mungu Mwana = ndiye mwokozi.

3: Mungu Roho mtakatifu = ndiye mshauri.

Kwa hakika madai ya wakristo ya kwamba Yesu ni mwana wa Mungu, au ni Mungu, au ni sehem ya Mungu, yanapingana na yale yaliyoelezwa katika Taurati na Injili, kwasababu imeelezwa ya kwamba Mwenyezi Mungu hatoonekana na yeyote hapa duniani: "Naye Baba aliyenipeleka amenishuhudia. Sauti yake hamkuisikia wakati wowote, wala sura yake hamkuiona. " (Yohana 5:37).

" Ambaye yeye peke yake hapatikani na mauti, amekaa katika nuru isiyoweza kukaribiwa; wala hakuna mwanadamu aliyemwona, wala awezaye kumwona. Heshima na uweza una yeye hata milele. Amina " (waraka wa kwanza kwa Timotheo 6:16).

" Kisha akasema, Huwezi kuniona uso wangu, maana mwanadamu hataniona akaishi (Kutoka 33:20).

Tukiziangalia hizi dalili na nyinginezo kwa hakika mimi naona ajabu sana na kujiuliza maswali kwa ukweli na uaminifu vipi tunaweza kuoanisha maneno ya wale wanaosema ya kwamba Issa (Yesu) ni Mungu na dalili za kitabu kitakatifu zinazo elezea na kuthibitisha ya kwamba hakuna yeyote aliyemuona Mwenyezi Mungu wala kusikia sauti yake?!.

Je! Mayahudi hawakumuona Issa (Yesu) (Mungu mwana kama wanavyo itakidi baadhi yao) kipindi kile na familia yake au wafuasi wake na kusikia sauti yake?

Kwanini Taurati na Injili vinaeleza ya kwamba Mwenyezi Mungu hajaonekana na yeyote wala kumsikia, kisha tunaona ya kwamba Issa (Yesu) waliomuona na kumsikia sauti yake wanaitakidi kuwa ni Mungu au mtoto wa Mungu? Je! Kuna siri iliyojificha kuhusu ukweli wa Mwenyezi Mungu?

Taurati inaelezea kinyume cha hayo inanukuu kuhusu kauli ya Mwenyezi Mungu: " Sikusema kwa siri, katika mahali pa nchi ya giza; sikuwaambia wazao wa Yakobo; Nitafuteni bure; Mimi, Bwana, nasema haki; nanena mambo ya adili (Isaya 45:19).

Ikiwa ndivyo uhakika uko wapi? Samahani soma dalili zilizo tangulia vizuri zaidi ya mara moja na ufikirie vizuri kwa umakini.

Na tuondoke pamoja katika msafara wa kutafuta ukweli kuhusu Mwenyezi Mungu katika kitabu kitakatifu na Qur-an Tukufu nikitaraji mtakubaliana nami kutokana na rai zenu na muono wenu baada ya kuzingatia kwenu Aya na dalili na kusoma kwenu kitabu hiki kwa mazingatio na kutafuta haki.

Kwa kuchunga mada tuliyonayo nitataja dalili bila ya kuweka nyongeza yoyote nataraji mazingatio kwa umuhimu wa mada hii.

MWENYEZI MUNGU NI MMOJA WA KWELI KATIKA (Agano la kale):

" Sikiza, Ee Israeli; Bwana, Mungu wetu, Bwana ndiye mmoja. (Kumbukumbu la torati 6:4).

"Je! Mwenyezi Mungu mmoja hajatuumbia roho ya maisha na kuturuzuku"?. (Malaki 2:15).

" Ninyi ni mashahidi wangu, asema Bwana, na mtumishi niliyemchagua; mpate kujua, na kuniamini, na kufahamu ya kuwa mimi ndiye; kabla yangu hakuumbwa Mungu awaye yote, wala baada yangu mimi hatakuwapo mwingine. Mimi, naam, mimi, ni Bwana, zaidi yangu mimi hapana mwokozi ". (Isaya 43:10-11).

" Bwana, Mfalme wa Israeli, Mkombozi wako, Bwana wa majeshi, asema hivi; Mimi ni wa kwanza, na mimi ni wa mwisho; zaidi yangu mimi hapana Mungu. "?. (Isaya 44:6).

" Hubirini, toeni habari; naam, na wafanye mashauri pamoja; ni nani aliyeonyesha haya tangu zamani za kale? Ni nani aliyeyahubiri hapo zamani? Si mimi, Bwana? Wala hapana Mungu zaidi ya mimi; Mungu mwenye haki, mwokozi; hapana mwingine zaidi ya mimi. (Isaya 45:21).

Je! Unakumbuka dalili nyingine kama hizo.

MWENYEZI MUNGU NI MMOJA WA KWELI KATIKA (Agano jipya):

" Na uzima wa milele ndio huu, Wakujue wewe, Mungu wa pekee wa kweli, na Yesu Kristo uliyemtuma (Yohana 17:3).

" Ndipo Yesu alipomwambia, Nenda zako, Shetani; kwa maana imeandikwa, Msujudie Bwana Mungu wako, umwabudu yeye peke yake " (Matayo 4:10).

" Sikia, Israeli, Bwana Mungu wetu ni Bwana mmoja nawe mpende Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote, na kwa roho yako yote, na kwa akili zako zote, na kwa nguvu zako zote. Na ya pili ndiyo hii, Mpende jirani yako kama nafsi yako. Hakuna amri nyingine iliyo kuu kuliko hizi. Yule mwandishi akamwambia, Hakika, Mwalimu, umesema vema ya kwamba Mungu ni mmoja, wala hakuna mwingine ila yeye ".

(Marko 12:28-33).

" Kwa sababu Mungu ni mmoja, na mpatanishi kati ya Mungu na wanadamu ni mmoja, Mwanadamu Kristo Yesu " (waraka wa kwanza kwa Timotheo 2:5).

"16 Na tazama, mtu mmoja akamwendea akamwambia, Mwalimu, nitende jambo gani jema, ili nipate uzima wa milele? Akamwambia Kwani kuniuliza habari ya wema? Aliye mwema ni mmoja. Lakini ukitaka kuingia katika uzima, zishike amri Akamwambia, Zipi? Yesu akasema, Ni hizi, Usiue, Usizini, Usiibe, Usishuhudie uongo." (Matayo 19:16-17).

Je! Unaweza kutaja dalili zingine zinazo thibitisha ya kwamba Mwenyezi Mungu ni mmoja na sio watatu?.

MWENYEZI MUNGU NI MMOJA WA KWELI KATIKA QUR-AN TUKUFU.

Amesema Yeye Mwenyezi Mungu Mtukufu:

(Sema: Yeye Mwenyezi Mungu ni wa pekee. Mwenyezi Mungu Mkusudiwa. Hakuzaa wala hakuzaliwa. Wala hana anaye fanana naye hata mmoja). (Surat Ikhlas 1-4).

(Na hatukumtuma kabla yako Mtume yeyote ila tulimfunulia ya kwamba hapana mungu isipo kuwa Mimi. Basi niabuduni Mimi tu). (Surat Ambiyaa 25).

(Kwa hakika wamekufuru walio sema: Mwenyezi Mungu ni wa tatu wa Utatu. Hali hakuna mungu ila Mungu Mmoja. Na ikiwa hawaachi hayo wanayo yasema, kwa yakini itawakamata adhabu chungu wale wanao kufuru). (Surat Maida 73).

(Hakika Mungu wenu bila ya shaka ni Mmoja).

(Surat Sswafaat 4).

(Au nani anaye uanzisha uumbaji, kisha akaurejesha? Na nani anaye kuruzukuni kutoka mbinguni na kwenye ardhi? Je! Yupo mungu pamoja na Mwenyezi Mungu? Sema: Leteni hoja zenu kama nyinyi ni wasema kweli). (Surat Nnamli 64).

Kwa hakika ujumbe huu (kumpwekesha Mwenyezi Mungu) ndiyo mada ya msingi ndani ya Qur-an Tukufu.

HITIMISHO

Kwa hakika dalili hizi na nyinginezo nyingi katika kitabu kitakatifu na Qur-an Tukufu zinaonyesha yasiyokuwa na shaka ndani yake ya kwamba Mwenyezi Mungu ni mmoja hakuna mwingine zaidi yake, kitabu kitakatifu kinasema: " Sikia, Israeli, Bwana Mungu wetu ni Bwana mmoja nawe mpende Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote, na kwa roho yako yote, na kwa akili zako zote, na kwa nguvu zako zote. Na ya pili ndiyo hii, Mpende jirani yako kama nafsi yako. Hakuna amri nyingine iliyo kuu kuliko hizi. Yule mwandishi akamwambia, Hakika, Mwalimu, umesema vema ya kwamba Mungu ni mmoja, wala hakuna mwingine ila yeye ". (Marko 12:28-33).

Na Qur-an Tukufu inataja jambo hili katika kauli yake Mwenyezi Mungu Mtukufu:

(Sema: Yeye Mwenyezi Mungu ni wa pekee). (Surat Ikhlas: 1).

Na kitabu kitakatifu hakitilii mkazo ya kwamba Mwenyezi Mungu ni mmoja tu bali kinatilia mkazo pia ya kwamba Mwenyezi Mungu ndiye muumbaji na muokoaji pekee, "Ninyi ni mashahidi wangu, asema Bwana, na mtumishi niliyemchagua; mpate kujua, na kuniamini, na kufahamu ya kuwa mimi ndiye; kabla yangu hakuumbwa Mungu awaye yote, wala baada yangu mimi hatakuwapo mwingine. Mimi, naam, mimi, ni Bwana, zaidi yangu mimi hapana mwokozi ". (Isaya 43:10-11).

Kwa sababu hiyo inabainika ya kwamba Uungu wa Issa (Yesu) au Roho mtakatifu au wengine tofauti na hao wawili hauna mashiko, wala dalili juu yake hawakuwa isipokuwa ni viumbe miongoni mwa viumbe wa Mwenyezi Mungu, hawana chochote katika maamrisho, wao si waungu wala hawafananishwi na Mungu. Hakuna kinacho fanan nae kwa mujibu wa kitabu kitakatifu na Qur-an Tukufu.

Kwa hakika Mwenyezi Mungu amewakasirikia Mayahudi kwa sababu ya upotevu wao na kuabudu miungu tofauti pamoja na Yeye, "Ikawa Israeli kujiungamanisha na Baal-peori; hasira za

Bwana zikawaka juu ya Israili" (Hesabu 25:3), na akaharibu Mussa (s.a.w) ndama yao ya dhahabu.

Kwa upande mwingine wamepata adhabu na mateso baadhi ya wakristo waliokuwa wakimpwekesha Mwenyezi Mungu, yote hayo ni kwasababu wameamini tauhidi ya Mwenyezi Mungu na wakakataa kubadilisha mafundisho sahihi ya kumpwekesha Mwenyezi Mungu ya Nabii Issa (s.a.w) na wakakanusha uzushi wa utatu mtakatifu ulioanzishwa na Paulo na wafuasi wake.

Muhtasari wa maneno Mwenyezi Mungu amemtuma Adam na Nuuh na Ibrahim na Mussa na Issa na Muhammad (s.a.w) kuwalingania watu katika imani ya kumuamini Mwenyezi Mungu na kumtakasia ibada yeye peke yake hana mshirika wala mwenza utakasifu ni wake. Huu ndio ujumbe wao wote.

Mungu wa kweli ni mmoja tu muabuduni peke yake.

Kwa hali namna ilivyo ni kwamba ujumbe wa Manabii na Mitume ni mmoja kwa sababu hiyo na dini yao ni moja. Ikiwa ndivyo ni ipi dini ya hao Manabii na Mitume?.

Kwa hakika kiini cha ujumbe wao kinasimama juu ya "kujisalimisha" kwa Mwenyezi Mungu, hili ndilo neno linalobeba maana ya "Uislam" na ndivyo lilivyoeleweka katika lugha ya kiarabu.

Na kwa hakika Qur-an imaetilia mkazo ya kwamba Uislam ndiyo dini ya haki kwa Manabii wote wa Mwenyezi Mungu na Mitume wake, na tunaweza kufuatilia uhakika huo uliopo ndani ya Qur-an kwenye kitabu kitakatifu pia. (Tutafatilia uhakika huo katika kitabu kitakatifu kijacho akipenda Mwenyezi Mungu).

Na mwisho kabisa, ni wajibu juu yetu kwa ajili ya kupata ufupisho wa maneno kuupokea ujumbe huu na kuuamini kwa ukweli na ikhlas. Lakini jambo hili halitoshi peke yake! Bali ni wajibu juu yetu pia kuamini Manabii wote wa Mwenyezi Mungu na Mitume wake (na inakusanya imani hiyo kumuamini Mtume

Muhammad s.a.w), na kufuata mwongozo wao na kuufanyia kazi hii ndio njia ya kupata maisha mazuri ya milele.

Ewe unayetafuta uhakika kwa ukweli kabisa na kutaka kuokoka yakupasa kutafakari katika jambo hili na kuzingatia sasa hivi kabla muda haujapita. Kabla hujafikiwa na umauti ghafla! Nani anajua lini ataondoka?.

Baada ya kutafakari na kuzingatia katika jambo hili muhimu sana na kwa akili yenye kudiriki na kwa moyo safi unaweza kuchukua uamuzi ya kwamba Mwenyezi Mungu ni mmoja hana mshirika katika Uungu wake wala mtoto, yapasa kumuamini yeye na kumuabudu peke yake na kuamini ya kwamba Muhammad ni Nabii na Mtume kama vile Nuuh na Ibrahim na Mussa Issa (s.a.w).

Na kwa sasa yawezekana ukatamka –ukitaka-maneno haya:

Ash-hadu an laa ilaha illa Llah wa ash-hadu anna Muhammada rasulu Llah. (Nakiri kwa moyo na kutamka kwa ulimi ya kwamba hapana Mola apasae kuabudiwa kwa haki isipokuwa Mwenyezi Mungu mmoja tu, na nakiri kwa moyo na kutamka kwa ulimi ya kwamba Muhammad ni mja wa Mwenyezi Mungu na Mtume wake).

Shahada hii ndiyo hatua ya kwanza ya kufanya kuelekea katika maisha ya milele na ndio ufunguo wa kweli wa milango ya pepo.

Na utakapokiri kufuata njia, ni juu yako kutafuta msaada kwa rafiki yako au jirani yako Muislam aliye karibu na Msikiti au kituo cha kiislam ili upate elimu zaidi.

Anasema Mwenyezi Mungu Mtukufu:

(Sema: Enyi waja wangu walio jidhulumu nafsi zao! Msikate tamaa na rehema ya Mwenyezi Mungu. Hakika Mwenyezi Mungu husamehe dhambi zote. Hakika Yeye ni Mwenye kusamehe, Mwenye kurehemu* Na rejeeni kwa Mola wenu Mlezi, na silimuni kwake, kabla ya kukujieni adhabu. Kisha hapo hamtanusuriwa* Na fuateni yaliyo bora kabisa katika yale

yaliyo teremshwa kwenu kutoka kwa Mola wenu Mlezi, kabla haijakujieni adhabu kwa ghafla, na hali hamtambui).

(Azzumar: 53-55).

Na rehma na amani za Mwenyezi Mungu zimwendee Mtume wetu Muhammad bin Abdallah pamoja na familia yake na Maswahaba zake na watakao mfuata kwa wema hadi siku ya mwisho.